

International Training Program (ITP)

## On-site Education of Practical Languages for Area Studies

### Report in 2011

—Swahili, University of Nairobi, Kenya, 10 Aug. 2011 – 30 Jan. 2012—

Year of Enrollment: 2011

Graduate School of Asian and African Area Studies

Sayo Yamamori

#### **On My Swahili Language Training (Swahili)**

##### **Utangulizi**

Kuanzia mwanzoni mwa mwezi wa 8, mwaka wa 2011 mpaka mwisho wa mwezi wa 1, mwaka wa 2012, nilijifunza Kiswahili mjini Nairobi, Kenya. Kabla ya niende pale, nilijifunza Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kyoto.

Vile miaka miwili iliyopita, niliwahi kusoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa muda wa muhula moja. Kwa masomo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kyoto na uzoefu wa maisha ya Dar es Salaam, niliweza kusoma Kiswahili kwa kufaa.

##### **Uzoefu**

Wakati nilipohudhuria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nilisoma juu ya elimu ya Tanzania, hususani elimu ya kujitegemea chini ya sera ya Ujamaa kuanzishwa mwaka wa 1967 hadi katikati ya miaka ya 1980's. Wakati niliposoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Masomo yalifundishwa kwa lugha ya Kiingereza.

Nilijaribu kusoma lugha ya Kiswahili kabla ya mradi wa kubadilishana uzoefu wa wanachuo. Lakini matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maisha ya kawaida ni magumu zaidi kuliko niliyofikiria. Nilitaka kujiunga na darasa la Kiswahili, lakini kiwango cha darasa kilikuwa juu sana. Kwa hiyo, sikuweza kufaulu mitihani ya kujiunga.

Kwa bahati nzuri, karibu na wakati niliporudi Japani, uwezo wa kuelewa lugha ya Kiswahili uliongeza. Niliweza kwenda mahali po pote mweneywe kwa basi na niliweza kununua vitu vyo vyote nilivyotaka.

## **Masomo ya Kiswahili katika Jiji la Nairobi**

Wakati nilipoanza masomo ya Kiswahili, sababu ya uzoefu na uendeleaji wangu, niliweza kuongea Kiswahili kidogo. Kwa hiyo niliweza kuruka masomo ya msingi ya Kiswahili. Lakini bado kuna ukosefu wa masomo. Mwalimu wangu alinisaidia sana kukuza uwezo wangu. Alinishauri hata maisha ya binafsi mara kwa mara. Pia tulizungumzia mila za kiafrica na kijapani. Mazungumuzo hayo yaliongeza uwezo wangu.

Hadi mwisho ya mwezi wa 12, tuliendelea na masomo ya sarufi. Tangu mwaka mpya wa 2012, tulianza kusoma magazeti na kitabu cha Kiswahili kuhusu Chama cha Walimu wa Tanzania. Wakati wa likizo la Krismasi nilijaribu kusoma kitabu hicho. Lakini nikashindwa. Lakini mara moja nilikwenda darasani, walimu walinifundisha kwa urahisi. Nilishangaa nguvu ya ualimu.

Tangu wakati huo, nilijaribu kutafuta maana ya maneno mapya kama kila siku baada ya darasa. Mara kwa mara nilijaribu kusoma magazeti pia. Nafikiri iliongezea uwezo wangu sana. Pole pole, niliona kwamba naweza kusikia na kusoma maneno ambayo kabla ya kuingia shule hii sikuweza. Nilifurahia mabadiliko ya uwezo wangu wa kuelewa Kiswahili. Ilikuwa ni kama dunia nyingine imekuja mbele yangu. Kitabu nilichosoma kilihusu utafiti wangu, nikaweza kujifunza Kiswahili na masomo ya utafiti wangu pamoja. Bado ninahitaji kutumia kamusi kwa kusoma kamili, lakini ninaweza kufahamu namna ya kuchora mstari. Mwanzoni, sikutegemea kwamba masomo ya Nairobi yangu niwezesha hadi kuandika ripoti kama hii.

## **Hitimisho**

Ninawashukuru walimu na marafiki zangu walionisaidia katika masomo na maisha yangu. Ni matumaini yangu kuwa michango ya masomo ya lugha ya yatasaidia vijana wengine kwa uzoefu huo. Nitaendeleza changamoto kwa ajili ya sitapoteza niliyofundishwa na watu wote. Asanteni sana.